# MKE&MALI

# KWA

# ALIYEOKOKA

# KABLA YA NDOA

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha MKE NA MALI KWA ALIYEOKOKA . Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

MKE NA MALI KWA ALIYEOKOKA

1.Mke?……………………………………………………………..

2. Mke au rafiki (Nyoka atamdanganya– eva)?……...

3. Mke mwema kwa maono ya mume…………………..

4.Mke mwema & mume (Maono)............................….

4. Mke mwema (upendo na furaha)……………………..

5. Mke mwema (Sauti ya Mungu)...........................….

6. Mke  (wa tamaa yako)...........................................

7.Mchumba => mke (Usifanye uasherati)………………

8. Mali kutoka kwa Baba wa mbinguni…...................…

9.Mambo ya kuzangatia unapooa mke...................…..

10.Sifa ya Mke na Mume afahayo ktk ndoa………………

11.Talaka.......................................................................

12.Maombi Ya familia……………………………………………

13.Kuokoka……………………………………………………………

14. Mwisho…………………………………………………………

# 1. MKE?

Mke ni msaidizi wa kufanana na Mwanaume.Mwanamke ametwaliwa kwa mwanaume.

**Mwanzo 18**

"Bwana Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye."

Mke na mume ni mwili mmoja===>Mtu kamili au Binadamu.

**Mwanzo 2:21-25**

Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. Adamu akasema, Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume. Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja. Nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mkewe, wala hawakuona haya.

**Msaidizi**

Kazi ya Adamu ilikuwa bila ni kuilima ardhi ya bustani na kupanda ila akichoka mke ambaye alimsaidia.

**Mwanzo 5**

"hapakuwa na mche wa kondeni bado, wala mboga ya kondeni haijachipuka bado, kwa maana Bwana Mungu hajainyeshea nchi mvua, wala hapana mtu wa kuilima ardhi; "

**Mwanzo 2:7 – 8** Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai. Bwana Mungu akapanda bustani upande wa mashariki wa Edeni, akamweka ndani yake huyo mtu aliyemfanya.

## 2.MKE==>RAFIKI

Ee Mtu wa kimataifa uliyeokoka Huyo ni Mke anayeletwa kwako kama ambaye hujaoa baada kupata maono ya kufukuzwa usiku ukiwa umelala na kupita ktk majaribu ya kujaribiwa na shetani na kuokoka yaani bila kutenda dhambi.

Ukikutana naye wewe uliyetakiwa kuoa hutapewa maono juu yake ila yeye atapewa maono juu yako. Ukipokea unaweza kupoteza baraka zako na kuondolewa ktk kusudi la mungu utafanya dhambi ya uasherati kabla ndoa na hiyo ndoa kutokufanikiwa. Mke wa namna unaweza kukutana naye ktk wokovu ukweli si mke ni rafiki.

Unapaswa kumkataa na kutokumpokea na umchukulie kama rafiki ili usiwepo usiano wa ndoa au uchumba. Maana ukimpokea maisha yako ya wokovu yanaweza kuharibika na ukanyang'anywa muda wa kumtumikia Yesu kama Bwana.

Rafiki huyo aliyeokoka ukimpokea kama mke kwa yeye ndiye amepata maono wewe mwanaume hujapata bali uliona nyoka ujue shetani atakudanganya kwa kutumia huyo mwanamke ukiwa uhusiano naye kwa kufanya dhambi ya uasherati kama alivyomdanganya Adamu kwa kumtumia Eva na Adamu akaasi agizo la mungu na ujira wake ni laana na kifo.Kama utumishi ndani yako atakubali kuwa msaidizi bali utadumaa kiutumishi na kumwacha kumtumikia mungu wako shetani aweza kumtumia kunyang'anya ili haki uliyokuwa ukimpa mungu kumtumikia na kumtafakari Yesu kumpa yeye huyo mwanamke. Ukiwa mume hujapata maono juu ya huyo wala kusikia sauti ya Mungu wako anasemaje juu ya rafiki usimpokee kabisa.Lakini pia ukiona ktk maono kama ya kufukuzwa nyoka huyo ni shetani anakutafuta kaa ktk maombi ya mfungo Yesu akuokoe ktk saa kujaribiwa kwako anakuja kwako akutoe ktk imani ya wokovu kwa kukudanganya kwa hila na uongo ili utende dhambi na kuacha kuitumikia kweli ya Yesu iliyomo ktk biblia na kukufanya uache kutumika utumishi wa Yesu ndani yako

## 3. MKE==>RAFIKI

Ukweli kuota unafukuzwa na nyoka jitahadharishe Shetani atakuletea mke mwenye VVU ila utamtambua na kukuharibia wokovu kwa kukudanganya huyo mke si mke bali rafiki ila anaweza akawa amepata maono ya kukuona wewe akiwa anaomba mume kabla kukutana naye.Chamngaka ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ukajifunge mshipi kiunoni ukiona na kudumu ktk maombi Yesu aliyemshinda nyoka yaani shetani akuokoe na saa ya kujaribiwa kwako kama utapata maono ya kuona nyoka yaani shetani usiku ukeshe ktk maombi ya kumsihi Yesu akue usimtende dhambi utakapojaribiwa lakini pia ufahamu kuona nyoka ktk maono usiku ukiwa umelala kwa uweza wa roho mtakatifu msaidizi aliye ndani ujue shetani anakutafuta akupe VVU kataa kufanya uasherati na mwanamke yeyote unakutana naye ktk wokovu ujue maisha yako yapo hatarini.

**Maono ya nyoka===>VVU=====>Rafiki sio Mke**

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka usiwe mjinga kupita kiasi napenda ufahamu mambo hayo ili usiwe mshamba ktk wokovu. Mume ndiye anayeoa wala si mke hivyo kwa habari ya mke Mungu akitaka kukupa mke atasema nawe mwanaume kwa kumtumia roho mtakatifu aliye ndani yako kusema nawe au kukuonesha sura na umbo la mwanamke anayetakiwa kuwa mkeo usiku umelala au mchana mwanamke wenyewe anayetaka kukupa kuwa mke ni kanisa lako unapoabudu au usiloabudu la waliokoka. Ikitokea mwanamke umepata maono ya kuona mume ukutana naye usimwambie mpaka mungu atakapompasha habari juu yako ukae kimya usimwambie.

# 4. MKE==>RAFIKI

Kupewa maono mke na mume kunyimwa ukimwambia huyo mume akakupokea bila ya yeye kumara maono au kusikia sauti ufahamu maana huyo mke ni sawa na amekuoa ktk maisha ya ndoa hatakataa kukutii ktk mazuri unayomuamuru atataka umtii yeye. Wewe umekuwa kama mke yeye amekuwa kama mume.Itazame hii siri syo nyepesi kuifahamu labda usome biblia vizuri. Huyo mwanamke atakuwa na upendo na kukufurahia ilitakiwa iwe sifa yako mwanaume umpende mke na kumfurahia . Pia wewe mwanaume utakuwa mwenye kumtii mke kwa hofu  ya mungu akikuamuru jambo lolote unaloona machoni pako ni jema unalitenda kwa upendo ili usimpoteze ila ukimuamuru wewe jambo lako jema anakuzalau au kulipuuza anakataa kukutii.

Maombi ya mkesha binafsi na kufunga usiku na mchana ukipinga shetani asikudanye haijalishi mbinu atakazotumia kuja kwako kama na mtu au ugonjwa au yeye mwenyewe mungu akupe ushindi wa Yesu ambaye hakutenda dhambi wala kudanganywa na shetani ktk wokovu wake .

Ukiona Nyoka omba maombi ya kuepushwa VVU  pia omba usikosee kuoa na mungu akuepusha na mwanamke si mkeo na dhambi ya uasherati.Dumu ktk hayo maombi mpaka Roho atakushuhudia umeshinda nguvu ya huyo nyoka yaani shetani ktk ulimwengu wa roho jihadhari dhambi si uasherati yupo ili audanganye moyo wako utende dhambi.

# 5. MKE MWEMA KWA MAONO YA MUME

Mke mwema kutoka mungu unapewa mume aliyekuwa anaomba mke kwa oneshwa na mungu usiku akiwa amelala au mchana ktk maombi,ibada au kazi n.k . Mume ndiye anayepewa maono na Mungu mke si lazima

Mke mwema wa aina hii ambaye mume umemwomba vigezo vya kiroho na kimwili anakuwa navyo vyote kama uliweka vigezo ktk maombi yako.

Wakati mwingine anaweza ukamkuta hana kigezo cha kimwili ulichoomba hayo ndiyo macho yako yawezekana anacho kitajitokeza baadaye sana na tena utasema kumbe nisingemkataa au nashukuru bora nilivyompokea.

Wakati mwingine unachelewa kupata mke kwa sababu ya vigezo vyako vya mwili unavyomwambia Mungu ktk maombi.

Mke mwema huyu mungu humleta kwako mume kama majibu ya maombi yako.Mume ukioa mke wa aina hii kutengana hakupo unatakiwa ndoa yako ifanane kama ile ya Adamu na eva walivyoishi pamoja baada ya kuondolewa Edeni na mungu ukweli hawakutengana wala kutalakiana maana ukimtaliki mkeo unafanya kuwa mzinzi maana huangukia ktk vishawishi vya tamaa ya mwili na alishazoea ndoa. Pengine haipiti wiki bila kufanya tendo la ndoa ulipokuwa pamoja ktk ndoa.

## Mathayo 19:3—6

"...Je! Ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu? Akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, **aliwaumba** mtu **mume** na mtu **mke,** akasema, Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa **mwili mmoja?** Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe. Wakamwambia, Jinsi gani basi Musa aliamuru kumpa hati ya talaka, na kumwacha? Akawaambia, Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu; lakini tangu mwanzo haikuwa hivi. Nami nawaambia ninyi, Kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa ni kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini; naye amwoaye yule aliyeachwa azini. Wanafunzi wake wakamwambia"

## 6. MKE MWEMA &MUME (MAONO)

Mungu hukuletea mke mwema uliyeomba ambaye amempa maono kabla ya kukutana naye na anakupa maono wewe mume uombaye kabla ya kukutana naye. Mkukutana mume ukamjulisha ulikuwa unaomba mke kwa mungu akaonyesha sura yake na umbo lake ndiwe wewe naye atakuambia nami ilikuwa naomba nipewe mume nilionyeshwa wewe kabisa sura ndiyo hiyo hiyo.

Kinachofuata ni furaha kwa kuwa wote mlikuwa mmejiandaa kuingia ktk ndoa.Kumshukuru mungu na mume kwa ulikuwa umejiandaa kufanya mikakati ya kuoa kutoa barua ya kujitambulisha kwa familia mke dhamira yako ya kutaka kuoa ili wakujibu kwa kukupangia mali inayotakiwa kutoa ili familia ikukabidhi binti yao na kukutambua wakikukubali family itajibu barua yako itakayokutambulisha wanahitaji mali kiasi gani? Mfano shs 50,000/= au Tshs. 3,000,000. Ukilipa unafanya mikakati ya kutangaza ndoa na kuoa.

Ijapokuwa ni mkeo huyo ulioneshwa na kuhakikishiwa na mungu kwa njia ya maono na yeye pia kupewa usifanye naye uasherati usije ukaingiza tabu ktk ndoa yenu kwa ku mkasirisha mungu. Mke anaweza kupata mimba kabla ya ndoa ni aibu ukienda kuoa mke ana mimba au umezaa naye wengi utafikiri mioyo inasema umefanya uasherati kabla ya ndoa.

Onyo ee mwanamke uliyeokoka uliyepata mume wenye utayari kukuoa na aliyepata maono juu yake nawe pia ukiwa bikira mfiche asije akalala nawe kabla ndoa na kumkosea mungu na mwanaume ukiwa hujalala na huyo ndiye wa kwanza ni mkeo mfiche usimwingilie kabla ya ndoa.

# 7. MKE MWEMA(UPENDO&FURAHA)

Imeandikwa **Efeso 5:25**

“Enyi waume, **wapendeni** wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; “

**Mith 1:18**

“Chemchemi yako ibarikiwe; Nawe **umfurahie** mke wa ujana wako.”

Mke mwema huletwa na mungu kwa mume huyu mume kila ukimuona au ukikutana naye ktk ibada au maombi au kwa habari ya jambo lolote la kikanisa moyo wa hujaa upendo na furaha ya roho mtakatifu naye hukushudia moyoni mwako ni mke bila maono kupewa maono na mungu.

Utaumtambuaje huyo ni mkeo huja na baraka utashangaa maongezeko ktk kipato chako hutapata shida ktk kumuoa hajaja hakuletee tabu bali ukimkaribia taabu zinaondolewa unainuliwa kiuchumi hata kabla ya hujamuoa.

Nimekuandikia haya Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka u kijaona ujaoa usikosee kuoa hasa kumtambua mke mwema anayetoka kwa mungu kwa kumwomba mungu wakati mwingine bila kumwomba ila kutokana umefurahisha moyo wa mungu na mungu ameamua kukubariki sikuzote usimpokee yule rafiki ambaye nimekwambia habari zake yeye huletwa kama mke ila amebeba VVU au ameletwa shetani kukuharibia baraka zako na kukutoa ktk kusudi la Mungu.Jifunze ukipewa mke uwe umemlipia mali au la ila umjitambulisha kwa wazazi wake nenda kapime naye VVU pia epikuka kufanya naye tendo la ndoa kabla ya ndoa mpime pia uzazi wote wawili mapema mkiwa mnaanza safari yenu kuelekea ktk kufunga ndoa siyo mwishoni majuto hayatakiwi usije ukasema nimepoteza bure au la ningejua...? Usisahau kumshukuru mungu upato kitu chema mfano mke.

# 8. MKE MWEMA (SAUTI YA MUNGU)

Huyu ni mke mwema kutoka kwa Mungu ni Mungu atasema nawe utasikia sauti yake yenye msukumo ndani ya roho yako ikisema nawe juu ya mke na roho mtakatifu akishuhudia ni mungu ndiye anayesema nawe. Mungu atasema nawe kijana wa kiume bila kukupa maono kama ilivyo kawaida ya vijana wengi waliokoka na walio ktk maombi ya kuomba mke mwema kutokana na wokovu wao u safi mbele za Mungu na Yesu.

Mungu akitamka jina la mke ujue hilo jina lipo ktk biblia takatifu si nje ya biblia. Mke mwema mungu akimleta kwako huwezi kuwa na tamaa mbaya ya ujani ya mwili.

Utii wako kwa mungu ktk kutembea ktk kusudi lake na kufanya mungu kutafanya urithi mke huyo mwema. Ila ukikosea na kufanya uasherati na rafiki ukamsahau huwezi kumpata bali baraka yako itanyanywa na adui zako.

Siyo tu kufanya uasherati bali hata kumtamani ambaye siye na kutafuta kuona kuona sehemu ya siri ya mwanamke yeyote baada mungu kusema nawe utanyang'anywa na mungu wa manabii.

Ee mtu wa kimataifa uliyokoka umeelewa u kijana yupo mke mwema mungu aweza kukupa ili kukusaidia kuishi ktk kusudi lake kwa kuzifurahia baraka zake epuka uasherati utampata kusahau sauti ya mungu ilichosema nawe kuhusu mke ni dhambi endapo roho mtakatifu hatakukumbusha hilo si kosa lako usijihukumu. Ila ukimpoteza ujue mungu hakupi mwingine mungu hakuumba eva wawili kwa ajili ya Adamu.

## 9. MKE (WA TAMAA YAKO)

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka kumbuka kabla hujaokoka ulipokuwa u mwenye dhambi ukifuata tamaa zako za mwili. Ulikuwa ukipenda kufanya nao uasherati wanawake pengine wembamba,wanene,weupe au wazungu kadri tamaa yako inavyowaka ulikuwa huwezi kujizuia maana huna imani inayokuia yenye uweza na hofu ya mungu ni ndogo kama si kuokoka nao ungeoa kama wenzako wenye dhambi  na yule mwanamke ungelimwita mke.

Una huo uzoefu na umri umefika wa kuoa nawe umeokoka na tazama kwa kuwa u mtu mwenye elimu ya hekima ya kibinadamu na umejiandaa una kila kitu cha kumhudumia mke kwa uzoefu wako ukimuamua kutqfutq mke umpendaye ktk kwa si sifa umbo la mwili huwezi kushindwa kupata anayefanana na wale uliowapendana zamani ungalimwenye dhambi hukuweza kuwaoa kwa sababu ya ujana.

Una mchagua mwenyewe kanisani na kumwoa kwa  ndoa ana sifa za mwili za wanawake uliokuwa unawependa sana ulipokuwa mwenye dhambi kabla hujaokoka.

Hiyo mke ni chaguo lako unapaswa kutomtendea na kumuwazia mabaya kama ulivyowatendea wale uliokutana nao uliowapenda wa kufanana naye kabla hujaokoka.

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka mke wa aina hii mkikaa miaka zaidi ya 12 bila ya wewe komkosea mungu kwa kwenda nje kwa kuwa ametosheleza udhaifu wako mshukuru Mungu maana shida ipo kwako.Uwe na hekima kama ni mshamba.

## 10. MCHUMBA==>MKE(UASHERATI)

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka na uliyejiandaa kuoa unaweza kuomba mbele mbele za mungu akupe mchumba ambaye ukayeishi naye kwa muda kwenye mahusiano baadaye ungelitaka awe mke baada ya kuona anafaa kuwa mke.

Roho mtakatifu aliye ndani yako ni kweli na kweli ukimwomba mchumba anakupa mchumba ujiwekee 100% moyoni ndiye utakayemwoa uchumba unaweza kuvunjika wakati wowote ukitaka huyo mchumba awe mke usifanya naye **uasherati** la hataweza kufikia kwenye lengo la kuwa mke kwa kuwa mmeokoka huo uchumba utavunjika.

Kuna watu waliokoka husema nimepata wachumba watatu au zaidi wote wameniacha. Kosa lako mwanamke ni hili mtu mume ajaye kwako anataka kukuoa Muulize wewe **uliomba mke au mchumba?** Akisema mchumba jitahadhari usifanye naye naye **uasherati ,** akisema mke mwambie afuate utaratibu vizuri naye usimpe mwili wako kabla ya ndoa.

Ikiwa ni mwanaume uliyeokoka kila ukipata mchumba kwa kumuomba mungu anayetaraji umuoe anakuacha ufahamu kosa lako la kwanza uliomba **mchumba** si mke, la pili ukipata mchumba unakimbilia kufanya naye **uasherati** na mungu mungu anakunyang"anya huyo mchumba maana umemkosea.

Kama umjiandaa kuoa na una kila kitu cha kumhudumia mke usiombe mchumba omba mke utafikia lengo lako la kufunga ndoa naye.

# 11.MALI KUTOKA KWA BABA WA MBINGUNI

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka yapo iko mali uwezayo kumwomba Baba wa mbinguni baada ya yeye kukupa mke mwema siyo mchumba kabla kumuoa kwa ndoa kanisani:=>

1) Mali kumwolea huyo mke na inayokamilisha mambo yote ya ndoa. **( Mwanzo 24 )** 2)Nyumba ya kuishi wewe na mkeo

3)Mali ya kumhudumia mkeo na hata watoto ataokupa.

**Mith 19:14** "Nyumba na mali ni urithi apatao mtu kwa babaye; Bali mke mwenye busara, mtu hupewa na Bwana. "

Yesu ndiye pekee aliyemwita mungu ni Baba yake. Ndiye aliyefundisha kumwomba baba yake kwa jina lake naye atalitenda. Kama sisi tu warithi pamoja na Yesu tunapozaliwa mara pili yaani kwa maji ni ubatizo na roho ni kujazwaa roho mtakatifu huko ni kuokoka hivyo tuliokoka ni wana kama Yesu mbele za mungu tuna haki ya kumwita mungu Baba yetu maana ametuzaa kwa roho mtakatifu.

Ee mtu wa kimataifa uliyeoka mungu amekupa mke bado hujafunga naye ndoa na unajishughulisha funga na kumwomba Baba wa mbinguni akupe Nyumba na Mali urithi wako kutoka mungu kwa ajili kumwolea mke na kumhudumia pamoja na nyumba ya kuishi na mkeo na atende hivyo kila akubarikipo kwa kukuongeza ktk mali na nyumba za kumpa mtoto au watoto aliokubariki wakiua.

Sehemu ya maombi unayotakiwa kuwa na hata ukioa ni kumwomba Baba yako wa mbinguni akupe nyumba na mali kuhudumia familia aliyokupa. Ukisoma **Mith 13:22** Wapo watu wema na wenye dhambi wamewapa watoto wao urithi. Bali ukisoma **Marko 10:18** Yesu hakuna anapita mungu kwa kutenda mema. UKimwomba mungu kama Baba urithi wa mali na nyumba Ee mtu kimataifa uliyeokoka ufahamu atakupa hasa wewe aliyekupa mke ndio upo ktk mchakato wa kuoa au wewe uliye ktk ndoa na una familia,

# 12. MAMBO YA KUZINGATIA UNAPOOA MKE

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka yapo mambo ya kuzingatia unapotaka kuoa; kuna mambo ya mungu,mambo ya mwili na mambo ya rohoni.

**<u>1) Mambo ya mungu.</u>**

Kupitia nabii Musa mungu aliwaambia wanaume wasitwa mke wa mataifa bali waoe waisrael I wenzao kwa wanawake vivyo waaitwaliwe na waume wa mataifa. Kumbuka Israeli iliyokuwa inaongozwa na mungu kwa kutumia manabii na wafalme waliomtii mungu inafanana na kanisa la waliokoka. Kam umeokoka u kijana hujaoa au olewa hutakiwi kutwaa mke au mume mwenye dhambi ambaye hajaokoka. Ni vizuri akiwa wa kanisa unapoenda kumwabudu mungu likiwa kanisa lako lipo mpaka nje ya nchi uwe na imani huyo mke mungu anaweza kukupa sio lazima awe wa nchi yako na wa nchi zingine ambalo kanisa lako lipo.

**<u>2)Mambo ya mwili</u>**

Yale yote uliyoomba mbele za mungu ukupe mke au mume mwenye nayo mfano mweupe,mwenye kitambi na mwenye pesa,mwembamba, mwenye uume wa nchi nne au nchi sita. Mke mwenye uwezo wa kutoshelezwa nchi nne au nchi sita. Asiye towashi tasa au mgumba ; asiye na ugonjwa wowote unaoweza kuzuia kupatikana kwa mtoto ktk ndoa., Aliyeishia darasa la saba au mwenye shahada. n.k

**<u>3)Mambo ya rohoni</u>**

Yale yote uliyoomba mbele za mungu ukupe mke au mume mwenye nayo mfano awe ameokoka ,mtakatifu,mtii kwa mume,mwenye usafi, mume upendo na kunifurahia,mke mwema na mwenye busara,anayempenda mungu,Mwenye kunia mamoja ktk mambo mema ya kifamilia na ya mungu pia. Ambaye hutatengana naye ukimwoa au kuolewa mpaka mmoja wenu afe. n.k

Hayo ndiyo mambo matatu ya muhimu unapotaka kuoa mke mwema

## 14. SIFA YA MUME NA MKE IFAHAYO KTK NDOA

Sifa ambayo mwanaume unatakiwa kuwa nayo ktk ndoa ni kumpenda na kumfurahia mke (kiroho) lakini pia uwe na uwezo wa kumhudumia mahitaji muhimu (kimwili) kama mavazi ,chakula, gari,nyumba,

“Enyi waume, **wapendeni** wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; “

**Mith 1:18**

“Chemchemi yako ibarikiwe; Nawe **umfurahie** mke wa ujana wako.”

Sifa ya mwanamke muhimu ktk ndoa ni utii kwa mume (kiroho) na za kimwili anajua mume.

**Efeso 5:22**

“Enyi wake, **watiini** waume zenu kama kumtii Bwana wetu. “

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka kama unajianda kuwa mke mwema au mume bora kaa ktk **maombi** mwombe Yesu akutengeze au akuumbie hizo sifa ktk roho yako yaani kwa mke utii kwa mumeo na upendo kwa mke na kumfurahia.

**NB:** Kwa mpakwa mafuta mwepuke shetani mke unayeletewa anayesababisha upako kuondoka ktk maisha yako au kudumaa kiutumishi si mzuri kwako baada ya kumpokea tu unaanguka naye ktk uasherati si mzuri kwako kabla ya kuja kwako ukaoneshwa unafukuzwa na nyoka huyo ni shetani huyo mke si mzuri kwako anawezekana ana VVU. Mke unayekutana naye kwa mara kwanza baada ya kufahamiana ukasahau kwenda kupima naye VVU si mzuri kwako.

Unatakiwa ukikutana mume,mke au mchumba baada ya kufahamia mwambie mkapime VVU kabla ya ndoa mkiwa kwenye mahusiano kama ya urafiki usije mkajisahau na kuangukia ktk uasherati mkiwa hamjapima ukajuta. Ukiwa peke yako u salama kama sikio sikia.

# 13. TALAKA

Talaka ni barua ambayo mume humpa mke kwa lengo la kutengana naye kwa muda kwa sababu fulani mfano uzinzi, uasherati, hajui kupika,hapendi ndugu, mchawi, mwizi, mchafu,si mtii kwa mume n.k

Yesu anasemaje kuhusu Talaka na ndoa kwa jumla? Sababu ipi Yesu anakubali unaweza kumtaliki mkeo.

**Mathayo 5.31**

“Imenenwa pia, Mtu akimwacha mkewe, na ampe hati ya talaka;

lakini mimi nawaambia, Kila mtu amwachaye mkewe, isipokuwa kwa habari ya **uasherati,** amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini. “

Ipo sababu moja Yesu alisema unaweza kumtaliki mke nayo ni **uasherati** peke yake si kila sababu. Athari za kumwacha mke kwa kumtaliki anamfanya kuwa mzinzi kivipi? Anakiwa hivyo bila kulala na mwanaume akilala naye azini nawe ukilala na mwanamke mwingine unazini mnatakiwa make hivyo hivyo bila kulala na wengine.

Ukisoma Mathayo 19:1-9 Yesu alitaka tukumbuke mungu alimwumba mtu mume na mke wawe mwili mmoja yaani Adamu na Eva na ndio wote walioa wanakiwa wawe hivyo. Mara nyingi sababu za wanandoa kutalikiana zinatoka na watu Yesu anasema anasema alichokiunganisha mungu  mwanadamu asiwatenganishe.Mume kataa  kumtaliki mkeo kwa sababu ya watu na maneno au matendo yao.Yesu anataka ukimwoa mke ukae naye siku zote mpaka kifo kiwatenganishe. Talaka ilikuja kwa sababu ya ugumu wa moyo yaani kutomwamini mung u hivyo uliyeokoka talaka si fungu lako maana wewe ni uaminiye haumo miongoni mwa wasiomwamini mungu.

## 13. MAOMBI YA FAMILIA

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka  yapo mambo ya muhimu ya kuomba wewe na familia ktk chumba cha ndani ya nyumba kama unayo ulichokitenga kwa ajili ibada au maombi ya kifamilia:=>

- Watoto wawe watii kwa wazazi
- Mke awe mtii kwa mume
- Mume uwe na upendo na kumfurahia mkeo
- Nyumba
- Mali
- Sehemu ulizowekeza mf : Mgahawa au kazini Mungu akubariki
- Ikiwa umebarikiwa kwa kiasi Fulani omba utajiri
- Mungu akupe watoto watakao watakaomtumikia mungu sikuzote za maisha yao duniani kwa kuokoka
- Watoto wafanye vizuri ktk elimu na kufikia kupata shahada
- Amani,furaha,upendo na haki ya Yesu itawale ktk familia
- Baada ya maisha ya wokovu mkutane makao ya Yesu mbinguni. n.k

Kumshukuru mungu ni muhimu baada ya yeye kukutendea mema yale uyaombayo na familia yako.Mshukuru mungu sadaka au kwa matoleo , mshukuru mungu kwa maneno ya kinywa chako.

## 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka  kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**

Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :


**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 35666

Mwenge DSM Tanzania



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034